THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

SCHOOL BASED ASSESSMENT

KISWAHILI

SEHEMU A

Zoezi 1 na 2

Gredi ya 5-2026

NAKALA YA MWALIMU

© 2026 The Kenya National Examinations Council

Sehemu A inatathmini Stadi ya Kusikiliza na Kuzungumza. Inajumuisha mazoezi matatu:

i. Mazungumzo ya ana kwa ana

ii. Ufahamu wa Kusikiliza

iii. Kusoma kwa sauti

Maagizo ya jumla

1. Wafahamishe **wanafunzi wote** kwamba mazoezi yote katika sehemu hii yatakuwa tathmini ya ana kwa ana. Kila mwanafunzi atakuwa na zamu yake ya kutathminiwa; mmoja baada ya mwingine.
2. Wafahamishe kwamba karatasi hii ina mazoezi matatu:
    i. **Mazungumzo ya ana kwa ana**
    ii. **Ufahamu wa Kusikiliza**
    iii. **Kusoma kwa Sauti**
3. Mwanafunzi aandaliwe kiti au dawati kutazamana nawe.
4. Tanguliza kila zoezi na umfahamishe mwanafunzi matarajio ya kila zoezi.
5. Mfahamishe mwanafunzi kukamilika kwa kila zoezi.
6. Tathmini umilisi wa mwanafunzi kwa mujibu wa mwongozo wa kutathminia. Weka rekodi ya matokeo ya tathmini.

© 2026 The Kenya National Examinations Council

ZOEZI 1A: MAZUNGUMZO YA ANA KWA ANA

Maagizo maalum

i. *Andaa mazingira mazuri ya tathmini kwa kumkaribisha mwanafunzi.*

ii. *Mwamkue na kumwomba akae.*

iii. *Jitambulishe kwake kwa kusema, 'Mimi ni mwalimu_____'.*

iv. *Muulize jina lake.*

v. *Anza tathmini kwa kusema,*

'Leo ningependa tuzungumze kuhusu huduma ya kwanza.'

1. Je, unafahamu nini kuhusu huduma ya kwanza?
   (Mwanafunzi ajibu)
2. Rafiki yako ameteleza na kutoka ngozi kwenye goti lake. Nitajie huduma ya kwanza utakayomfanyia.
   (Mwanafunzi ajibu)
3. Umeumia kidole ukiwa darasani. Hata hivyo, hakuna kisanduku chenye vifaa vya huduma ya kwanza darasani. Unadhani wenzako watafanya nini ili kukusaidia ?
   (Mwanafunzi ajibu)
4. Mtu anapotokwa damu baada ya kuumia anaweza kufungwa mahali alipoumia kwa kutumia kitambaa maalum. Je, kitambaa hicho kinaitwaje?
   (Mwanafunzi ajibu)

ZOEZI 1B: UFAHAMU WA KUSIKILIZA

Maagizo maalum

i. *Msomee mwanafunzi kifungu kifuatacho* ***mara mbili.***

ii. *Mjulishe kuwa atajibu maswali baada ya kusomewa kifungu mara ya pili.*

Mapambo ni vitu ambavyo hutumiwa kuongeza urembo kwa mtu. Vijana wengi siku hizi wanapenda kutumia mapambo ili kuonekana nadhifu. Wasichana hutumia mapambo kama vile poda kwenye uso, wanja kwenye nyusi za macho na rangi za kupakwa kwenye kucha. Pia, wao hupenda kutumia vito vya thamani kama vile herini au vipuli kwenye masikio na shanga shingoni.

Wavulana nao hawajaachwa nyuma. Wao hupenda kuvaa saa za mikononi, cheni za fedha shingoni na manukato ya kiume.

Hata hivyo, baadhi ya mapambo hayo huweza kutumiwa na vijana wa jinsia zote. La muhimu ni kuyatumia kwa njia inayokuza na kuonyesha maadili.

© 2026 The Kenya National Examinations Council

5. Kulingana na kifungu hiki, mapambo hutumiwa kufanya nini?
   (Mwanafunzi ajibu)
6. Kifungu hiki kinaonyesha kuwa kuna usawa kati ya wasichana na wavulana kwa njia gani?
   (Mwanafunzi ajibu)
7. Je, unadhani kutatokea nini iwapo vijana watatumia mapambo kwa njia isiyokubalika?
   (Mwanafunzi ajibu)
8. "Vijana wa siku hizi wanapenda kutumia mapambo ili kuonekana **nadhifu."** Nini maana ya neno **nadhifu**?
   (Mwanafunzi ajibu)

ZOEZI 2 : KUSOMA KWA SAUTI

Maagizo maalum

i. *Mfahamishe mwanafunzi matarajio ya Zoezi la Kusoma. (Zingatia mwongozo wa kutathminia Kusoma kwa sauti).*

ii. *Mpe mwanafunzi nakala atakayoisoma kwa sauti.*

iii. *Mwanafunzi anaposoma, sikiliza na kurekodi idadi ya maneno anayosoma kwa muda wa* ***dakika moja.***

iv. *Onyesha kwa mshazari* ***(/)*** *mahali mwanafunzi alipofikia kusoma* ***dakika moja*** *ikikamilika.*

v. *Mruhusu mwanafunzi kusoma mpaka mwisho wa kifungu.*

vi. *Pigia mstari maneno* ***yote*** *ambayo mwanafunzi atashindwa kuyasoma au kuyatamka vizuri.*

vii. *Rekodi idadi ya maneno ambayo mwanafunzi ameweza* ***kusoma kwa usahihi*** *kwa dakika* ***moja****. (Baada ya kuondoa yaliyotamkwa vibaya au/na aliyoshindwa kutamka)*

viii. *Rekodi viwango vya umilisi wa mwanafunzi kwa kuzingatia mwongozo uliopewa.*

ix. *Hakikisha una nakala ya kurekodia tathmini hii. (Iwe na majina ya wanafunzi wote.)*

x. *Ukiwa tayari kuanza tathmini, sema,*

''Sasa naomba unisomee kifungu hiki kwa sauti.''

© 2026 The Kenya National Examinations Council

Zainabu anapenda sana kupika. Siku moja, aliamua kupika chakula cha 10 jioni. Alienda sokoni akanunua vyakula mbalimbali. Alinunua mboga, ndizi na 20 samaki. Aidha, alinunua viungo vya kupikia vikiwemo vitunguu, nyanya na 30 iliki.

Jioni hiyo, Zainabu alipika kwa bidii na nidhamu. Alitumia 40 viungo jinsi alivyotazama kwenye mtandao. Alitumia viwango vya joto vilivyofaa 50. Alitaka kuhifadhi virutubishi vyote muhimu katika vyakula alivyovipika.

Kila mmoja 60 katika familia yake alivutiwa na harufu nzuri kutoka jikoni. Wakati 70 wa kuandaa chakula ulipofika, Zainabu alikuwa tayari. Aliwaita ndugu zake 80 ili waje kumsaidia kupanga meza.// Familia nzima iliketi mezani na kula kwa furaha. Wote walikula wakashiba. Waliupenda upishi wake ambao waliuthamini sana. Wote walimpongeza Zainabu. Zainabu aliwashukuru kwa kumpongeza.

© 2026 The Kenya National Examinations Council